BINT EL SUDAN
Perfume • Powder
Pomade • Deodorant

DEODORANT SPRAY
YA MARASHI
ASILI YA MAPENZI
HAKIKA
UTA FURAHI

FUJI FUJI FUJI FUJI FUJI

Wasafishaji mashuhuri wa picha za rangi za *FUJI* ulimwenguni sasa wanapatikana mjini Mombasa

Aina zote za picha za rangi zinachapishwa:

FUJI • KODAK • AGFA
SAKURA • COLOURAMA

KWA USAFISHAJI WA PICHA ZAKO ZOTE ZA RANGI HAKIKISHA UNAZITUMA KWA MITAMBO MIPYA YA KISASAS YA FUJI

Zungumza na *Riaz Alibhai* kwa simu 313589, Mombasa ama fika kwenye mitambo hiyo mipya ya *FUJI*, iliyo pakana na afisi ya *Coastweek*, gorofa ya kwanza ya jumba la Banki ya Grindlays, katika barabara ya Digo Road na Nkrumah road.

FUJI FUJI FUJI FUJI FUJI

POLE

MAMIA ya Waombolezi walihudhuria mazishi ya Bi. Mwana Sayyid Hassan katika Makaburi ya Langoni, Kisiwani Lamu mnamo Oktoba 2, mwaka huu. **(Aripoti Gray Phombeah).**

Bi. Hassan ni khalati yake Mhariri wetu wa Kiswahili, Bw. Abdulrahman Sheriff. Aliaga dunia asubuhi ya Oktoba 2 na kuzikwa jioni yake.

Bw. Sheriff aliondoka kuelekea Lamu siku iliyofuata na kwa niaba ya wafanyakazi wote wa **Coastweek,** *ninatoa rambirambi kwa Bw. Sheriff pamoja na familia yake.*

Napenda kumhakikishia Bw. Sheriff kwamba sote katika **Coastweek** *tuko pamoja nayë katika wakati huu wa msibu mkubwa uliompata. Mungu atamueka mama yetu Mahala Pema Peponi, Amin.*

Mbali na msiba huo, Bw. Sheriff pia alifiwa na Khali yake Marehemu Abdallah Soud aliyeaga dunia nchini Tanzania na kuzikwa mjini Malindi mnamo Oktoba 1.

Hatuna budi pia kutuma risala zetu za rambirambi kwa familia ya Bw. Sheriff na jamaa ya Marehemu Bw. Soud. Mungu atamueka Mahali Pema Penye Wema, Amin.

BW. SHERIFF

BW. ISAAC NYARANGI Ondieki anayefanya kazi katika kampuni ya Bata Shoe (K) Ltd. Limuru akimvalisha pete Bi. Rose Nyaboke Nyabunga anayefanya kazi Kenya Posts & Telecommunications, Mombasa wakati wa harusi sherehe za arusi yao iliyofanyika mapema mwezi huu. Kulia kabisa na kushoto ni Bw. na Bi. Simion Tongi na Reg. alikuwa Bw. W. K. T. Richu. PICHA: LAWRENCE MWANTHI

Vijana Sote Tuchangamke — Asema A.M.S. Bathawab

na Abdulrahman Sheriff

VIJANA wana wajibu wa kujifundisha kila aina ya ufundi ili wainukie wakiwa wana ujuzi wa kutosha wa kuendeleza maisha yao ya baadaye. Hayo yalisemwa na Abdallah Mohammed Said Bathawab anayeendesha biashara ya hoteli kisiwani Lamu.

Kijana huyo wa miaka 30 alikuwa akizungumza na *Coastweek* kuhusu jinsi alivyojiendeleza hata akaweza kushikilia ujuzi aliokuwa nao babake ambaye alifariki miaka michache iliyopita.

Katika harakati za kupeleleza jinsi vijana wa Lamu wanavyojiendeleza, nilijaribu kumdadisi Bathawab kuhusu maisha yake ya utotoni na jinsi alivyoinukia hadi akafanikiwa kuendesha biashara hiyo.

Bathawabu alisoma katika Shule ya Msingi ya Lamu na baadaye akasafiri hadi Nairobi ambapo alijifundisha jinsi ya kutenegeneza mashini za barafu Alifanikiwa kupata shahada ya Kwanza.

Hata hivyo, Bathawab hakuweza kuendelea na shughuli hiyo ya ufundi wa mashini za barafu alirudi nyumbani apate kumsaidia babake katika kuendesha hoteli yao iliyokuwa maarufu ikiitwa Zanzibar Hotel.

Kijana huyo alimsaidia babake na kujifunza mengi kuhusu upishi wa vyakula mbali mbali. Alioa na kwa wakati huu ana watoto wawili ambao bado ni wadogo.

BW. ABDALLAH Bathawabu ni mmoja tu ya vijana wa Lamu wanaoinukia na kujiendeleza katika mambo ya biashara. Wakati ukifika, nitawaletea historia fupi ya vijana wengine waliojiendeleza kimaisha.

Ilikuwa mwaka huu, Bathawab alifungua hoteli yake mwenyewe na kuipa jina la Sabrina Restaurant. Hoteli hiyo ilifunguliwa rasmi mnamo Mwezi wa Mei katika mtaa maarufu unaojulikana kama Langoni.

TAMBUU

Hoteli hiyo imeshakuwa maarufu hasa kutokana na watu wengi kufika mahala hapo ambapo pembezoni "Tambuu" na mfanya biashara maarufu anayeitwa Hassan. Pia kuna mchezo huchezwa nao waitwa "Dhumna".

Bathawab alinambia kuwa amejifunza aina nyingi za chakula ambacho kinauzwa hapo hotelini kama pilau, wali mweupe, sima, taco salads, sandwich ya cheese, mapishi ya mayai aina mbali mbali na kadhalika,.

• BW. BATHAWAB

Ile hoteli ya babake ya Zanzibar Hotel sasa inasimamiwa na ndugu yake anayeitwa Sultan Bathawab. Abdallah alisema kuwa atajaribu awezavyo watoto wake wachukuwe ujuzi zaidi katika Utalii College.

Mzee Marehemu Babake ambaye alikuwa akijulikana maarufu kama Badi Bathawab alizaliwa Lamu mwaka 1921. Akaenda Zanzibar kwa muda kabla ya kurudi pamoja na *Waunguja* na kusoma masomo ya dini. Halafu akafungua hoteli hadi wakati wa kifo chake.

WAMPONGEZA DKT. OMAR HATIMY

ALIYEKUWA Mchezaji wa Taifa wa Kenya miaka ya nyuma, Saad Mohammed Oshan alituma risala za pongezi kwa Daktari Omar Hatimy kutokana na kuchaguliwa kwake kama Mwenyekiti wa Shirikisho la Soka tawi la Pwani.

Katika taarifa yake ya pongezi, Saad alisema, "Natoa pongezi nyingi kwa Dkt. Omar pamoja na kundi lake kwa ushindi walionyakuwa na nawaomba wafanye mabadiliko ya katiba ili kukuza hali ya mpira hapa Pwani.

Saad alikuwa mchezaji maarufu wa timu ya Mseto ya Mombasa, Pwani na pia aliwahi kujibwaga kiwanjani kuwakilisha nchi yetu kwenye mechi kadha za Kimataifa. Alikuwa akicheza kwenye sehemu za kujihami.

Naye katibu wa klabu ya Bantu Warriors, Sher Khan naye alituma risala za kumpongeza Dkt. Omar Hatimy pamoja ná wenzake kwa ushindi walioupata dhidi ya wapinzani wao.

Alisema Sher Khan, "Ushindi wenuumedhihirisha wazi kwamba timu za Mombasa zinataka uongozi bora na wa busara na ndipo wakaamua kwa hiari yao kuwarudhishia tena wadhifa muliokuwa nao".

Mwenyekiti wa Black Panther FC, Mohammed Hassan "Father Bom" naye pia aliwapongeza viongozi hao wapya na kuwaambia: "ni juu yenu kuona kuwa munavitumikia vilabu vyote bila ya mapendeleo yote".

Bw. Hassan aliwaomba viongozi hao wasikubaliane na machafu yoyote yatendeke kwani, "mukianza kuyasafisha, ndipo hali ya soka katikaPwani itarudia kwenye hali ya kuridhisha kama zamani".

DKT. HATIMY

BW. OSHAN



BW. SHER KHAN

Farucci

BINT EL SUDAN
Perfume • Powder
Pomade • Deodorant

MARASHI
ASILI YA MAPENZI
HAKIKA
UTA FURAHI

JISHINDIE VIATU MARIDADI VYA FARUCCI KWA MSHINDI WA KWANZA NA 'BINT EL SUDAN - GIFT PACK' KWA MSHINDI WA PILI NA WATATU ATAPATA ZAWADI YA FLANA YA FARUCCI

CROSSWORD No. 219

KWENDA KULIA:

1. Msimamizi wa wafanyi-kazi fulani. 6. Katika ua. 8. Mnyama adui wa kuku. 9. Pande la chungu kilichovunjika. 11. Jina la kike. 13. Aina ya ndege kama njiwa. 15. Kiungo cha maneno. 16. Chama chetu cha Kenya. 17. Imalizike. 18. Chagua. 19. Kwama, saki.

KWENDA CHINI:

1. Mmea wa matunda. 2. Ua la mtoni au katika ziwa. 3. Post Office. 4. Jumla ya michezo yote ya mazoezi ya viungo vya mwili. 5. Jina la kikikuyu. 7. Itangulize. 10. Afrika Masharika. 12. Jina la kigiriama. 14. Teketea. 16. Wingi wa ukuta.



JINA.......................................

SANDUKU LA POSTA...................

....

MAJIBU YA SHINDANO LA FUMBO LA KUJAZA MANENO No. 218

KWENDA KULIA: 1. MAGARI, 4. UK, 6. KUNGWAA, 8. LAMI, 9. TWAZUA, 12. IANA, 14. NA, 15. KIKOI, 16. DUNI, 17. KAA, 18. UKUNI *KWENDA CHINI:* 1, MAKUTI, 2. ANGAZA, 3. ILALA, 5. KILINDINI, 7. AA, 10. WANDA, 11. ANAUA, 13. UKUU, 15. KIU.

WASHINDI WA FUMBO LA KUJAZA MANENO No. 219

1. BI. JEDIDAH WAMBUI M. Sanduku La Posta 84216, Mombasa. 2 BI. REHEMA T. MASHA. Sanduku La Posta 93404, Mombasa. 3. BERTINA KALE KIAGO, Sanduku La Posta 87294, Mombasa.

Shindano la Fumbo la Kujaza Maneno:—

Uamuzi wa majaji utakuwa wa mwisho. Hakuna malalamiko yoyote yatakayokubaliwa. Kila baada ya wiki mbili, Mshindi wa kwanza atapata viatu maridadi vya Farucci; wa pili atapata 'Bint El-Sudan-Gift Pack' na watatu atajinyakulia flana ya Farucci. Shindano hili limedhaminiwa na *COASTWEEK* Limited Mombasa. Jawabu za fumbo hili lipelekwe kwa Mhariri *COASTWEEK* , S. L. P. 87270, Mombasa. Mwisho wa kutuma Majibu na jumatano, **October16,1985** saa, nne asubuhi.